

**Sheikh Swâlih as-Suhaymî amzungumzia Sheikh  
Falâh Ismâ'îl Mandikâr**

---

# Sheikh Swâlih bin Sa'd as-Suhaymî (*hafidhahullâh*)

## Kumuhusu Sheikh Falâh Ismâ'îl Mandikâr

---

*BISMILLÂHI AR-RAHMÂNI AR-RAHÎM*

Siku chache zilizopita, baadhi ya wajinga na wapumbavu walikuwa wakijigamba na kupayuka kumuhusu mtu aliyezingatiwa kuwa ni miongoni mwa watangulizi wa Salafi Da'wah kutoka Kuwait, ndugu yetu Sheikh Falâh bin Ismâ'îl Mandikâr, twamuomba Allâh amponye na ampe afya njema, sasa hivi akiwa London, muombeeni Du'ah apate shifaa'. Baadhi ya watoto, baadhi ya vijana, baadhi ya waliodanganywa, wanaandika makala [ya kuwatahadharisha watu dhidi yake] “musimsikize”, “mbwagani”, “hafai kusikilizwa huyo kwa sababu rafiki yake mmoja amezungumzwa habari zake”! Huu ni upumbavu! Huu ni upumbavu kamili!

Kuzungumza kuwahu ma-'Ulamâ', Mashayekh na wanafunzi wa ki-ilimu. Nyama ya mwanachuoni ni sumu, na sunnah ya Allâh kwa wale wenye kuwaumbua wao inajulikana kikweli. Kwahivyo, tahadhari na huku kuzungumza kuhusu heshima ya wanafunzi wa ki-ilimu na ma-'Ulamâ'. Hilo ni suala la hatari. Suala hilo ni la hatari kubwa sana. Mtu akinijia mimi kutaka kunigeuza moyo wangu dhidi ya ndugu yangu, basi ni juu yangu kumkataa mtu kama huyo [yaani; mwenye kunijia akijaribu kuniingiza chuki] na kutomruhusu anipulizie sumu yake.

Mfasiri: Abu Farida Muhammad Awadh Salim Basawad

Sauti iliyorekodiwa inapatikana hapa <http://safeshare.tv/w/BNqshDrgve>